**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

**17 APRILI, 2026**

## YALIYOMO

*Ukurasa*

**YALIYOMO** .......... **iii**
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... **iv**
**SEHEMU YA KWANZA** .......... **1**
**1.0 UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Maelezo ya Awali .......... 1
1.2 Muundo wa Taarifa .......... 2
1.3 Msingi wa Uchambuzi .......... 2
1.4 Mawanda ya Uchambuzi .......... 3
**SEHEMU YA PILI** .......... **3**
**2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... **4**
2.1 Ufafanuzi wa Jumla .......... 4
2.2 Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 .......... 4
2.2.1.Fungu Na. 20 – Ofisi ya Rais (Ikulu) .......... 5
2.2.2.Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri .......... 6
2.2.3.Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. .......... 10
2.2.4.Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. .......... 12
2.2.5.Fungu Na. 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. .......... 14
2.2.6.Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma .......... 17
2.2.7.Fungu Na. 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa .......... 18
2.3 Tathmini ya Jumla ya Utekelezaji wa Bajeti .......... 19
2.4 Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 .......... 22
2.4.1.Miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) -Mradi Na. 6220. .......... 23
2.4.2.Ujenzi wa Jengo la Ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nyangh'wale-Mradi Na. 6203: .......... 25
2.4.3.Ujenzi na Ukarabati wa Jengo la Ofisi na Ghala Kuu la Nyaraka, Ilemela (Mradi Na. 6286 na Mradi Na. 6285) .......... 26
2.4.4.Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Jengo la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma .......... 28
2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati .......... 29
**SEHEMU YA TATU** .......... **29**
**3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** .......... **29**
3.1Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 .......... 30
3.1.1Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida .......... 30
3.1.2Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Miradi ya Maendeleo .......... 33
**SEHEMU YA NNE** .......... **35**
**4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... **35**
**4.1 MAONI YA JUMLA** .......... **35**
4.2 Ushauri Mahsusi Fungu kwa Fungu .......... 36
4.2.1 Fungu 30- Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri .......... 36
4.2.2 Fungu 67-Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma .......... 37
4.2.3 Fungu Na. 004-Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa .......... 38
**SEHEMU YA TANO** .......... **39**
**5.0 HITIMISHO** .......... **39**

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na: 1** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 20 ........................................ 6

**Jedwali Na: 2** Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi Februari, 2026 - Fungu 30 ........................................ 10

**Jedwali Na: 3** Fedha zilizopokelewa kwa Mwaka wa Fedha Julai, 2025 hadi Februari, 2026) - Fungu 32 ........................................ 11

**Jedwali Na: 4** Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 - Fungu 067 ........................................ 15

**Jedwali Na: 5** Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026-Fungu 094 ........................................ 17

**Jedwali Na: 6** Upatikanaji wa bajeti ya Matumzi ya Kawaida kwa mafungu yote........... 20

**Jedwali Na: 7** Upatikanaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mafungu yote kwa Mwaka 2025/2026 ........................................ 21

**Jedwali Na: 8** Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2025/2026 na Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2026/2027... 32

**Jedwali Na: 9** Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ........................................ 33

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (9**) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, muundo wa Taarifa hii umegawanyika katika sehemu kuu Tano ambazo ni: -

(a) Sehemu ya **Kwanza** inahusu maelezo ya jumla, ambayo pia inabainisha msingi na muundo wa Taarifa hii;

(b) Sehemu ya **Pili** inahusu uchambuzi wa Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

(c) Sehemu ya **Tatu** inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(d) Sehemu ya **Nne** inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Ofisi hii na Serikali kwa ujumla; na

(e) Sehemu ya **Tano** ni Hitimisho ikujumuisha shukrani.

## 1.3 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi na Maoni ya Kamati juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na masharti ya Kanuni ya 121(4) ikisomwa kwa pamoja na vifungu 6(2)(a) na 7 (1)(a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni na vifungu hivyo vimeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na

Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.4 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi huo, Kamati ilipokea, kupitia na kuchambua jumla ya mafungu saba (7). Mafungu hayo ni: -

(a) **Fungu 20**: Ofisi ya Rais, Ikulu;

(b) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

(c) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

(d) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(f) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na

**(g)** **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** katika kikao cha Kamati kilichoketi tarehe 10 na 24 Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliyohusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo iliwasilishwa na Waziri wa Ofisi hiyo **Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb)**. Kwa kuwa Ofisi hiyo haina bajeti ya makadirio ya makusanyo ya maduhuli, uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hiyo umeangazia maeneo makuu matatu ambayo ni: -

(a) Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;
(b) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na
(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 2.2 Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia hoja hii, Kamati ilizingatia Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Uchambuzi wa Kamati umeangazia mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida (*zinazojumuisha fedha za mishahara (PE), fedha za matumizi mengineyo (OC)* na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi huo kwa kila Fungu la Ofisi hii ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.1. Fungu Na. 20 – Ofisi ya Rais (Ikulu)

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu 20- Ofisi ya Rais (Ikulu) lilitengewa Shilingi **34,804,735,000.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **11,395,264,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi **23,409,471,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari 2026, Fungu 20 lilipokea jumla ya Shilingi **23,287,471,936.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 66.91** ya kiasi kilichoidhinishwa. Katika kiasi kilichopokolewa, **Shilingi 7,680,407,936.00** sawa na asilimia **67.40** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 15,607,064,000.00** sawa na asilimia **66.67** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Muhtasari wa mapokezi ya fedha hizo unaoneshwa katika **jedwali Na. 1** hapa chini.

**Jedwali Na: 1 Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 20**

| Fedha | Matumizi | Fedha Iliyoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | OC | 23,409,471,000.00 | 15,607,064,000.00 | 66.67 |
| | Mishahara | 11,395,264,000.00 | 7,680,407,936.00 | 67.40 |
| **JUMLA** | | **34,804,735,000.00** | **23,287,471,936.00** | **66.91** |

**C**

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kufanya tathmini ya kuangazia endapo upokeaji wa fedha ulifikia matakwa ya kibajeti katika wakati husika, mwezi februari Ofisi inatakiwa kupokea **asilimia 66.7** ya bajeti. Kwa mizania hiyo, tathmini inaonesha fungu hilo hadi februari, 2026 lilipokea **asilimia 66.9** ya bajeti iliyoidhinishwa. Hivyo basi, katika fungu hili hali ya upatikanaji wa fedha ilizingatia matakwa ya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Kupokelewa kwa fedha kwa kiasi cha kutosheleza kumewezesha Ofisi ya Rais kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria ipasavyo. Baadhi ya majukumu hayo ni kumuwezesha Mheshimiwa Rais kutekeleza kazi zake vyema kama mkuu wa nchi na amiri Jeshi Mkuu.

### 2.2.2. Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu 30 -Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **1,197,312,759,000.00.** Katika kiasi hicho, fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni shilingi **1,039,839,675,000.00**, (kiasi kinachojumuisha Shilingi **9,016,031,000.00** kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **1,030,823,644,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo). Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi **157,473,084,000.00,** ambapo **shilingi 88,934,306,000.00** ni fedha za Ndani na Shilingi **68,538,778,000.00** ni fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026, jumla ya **shilingi 775,164,080,621.34** zilipokelewa, sawa na **asilimia 64.74** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo kwa matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo ni kama ifuatavyo: -

**(a) Mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika,** kwa matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026 Fungu hili lilipokea Jumla ya Shilingi **693,409,775,963.67** sawa na asilimia **66.68** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo Shilingi **6,194,013,297.00** sawa na asilimia **68.70** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **687,215,762,666.67** sawa na asilimia **66.67** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, fungu 30 lilipokea fedha kwa kiwango kinachotakiwa katika kipindi husika kwani lilipokea **asilimia 66.68** ya fedha zilizoidhinishwa. Kupokelewa kwa fedha hizo kumewezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria.

Majukumu hayo ni pamoja na kuwezesha Taasisi zilizo chini ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya taasisi hizo ni Taasisi ya Mamlaka ya Serikali mtandao (e-GA), Wakala wa Ndege za Serikali, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Taasisi ya Uongozi, TAKUKURU, Baraza la Kumshauri Mheshimiwa Rais kuhusu chakula na Kilimo na Idara za Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

**(b) Mapokezi ya fedha za Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi februari, 2026, Fungu 30 lilipokea kiasi cha Shilingi **81,754,304,657.67** sawa na asilimia **55.44** ya fedha zilizoidhiniwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika kiasi hicho kilichopokelewa, **shilingi 55,661,087,102.00** sawa na asilimia **62.59** ya fedha za ndani, na shilingi **26,093,217,556.00.00**, sawa na **asilimia 44.57** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** kupokelewa kwa fedha za maendeleo kumewezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikiwemo kuendelea kuziwesha kaya maskini kupitia Shirika la maendeleo ya Jamii (TASAF), ujenzi wa majengo ya ofisi na nyumba za watumishi kwa ajili ya TAKUKURU kwa baadhi ya mikoa na wilaya na kutekeleza programu ya kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa. **Aidha, kwa miradi inayoendelea kutekelezwa, Kamati inaendelea kusisitiza uwepo wa usimamizi wa karibu ili miradi hiyo ikamilike kwa muda uliokusudiwa**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mradi wa kunusuru kaya maskini nchini, Kamati ilielezwa kuwa mradi unaotekelezwa kwa sasa ni wa awamu ya tatu ambao umefikia ukingoni. Ili kuendelea kuziinua kiuchumi kaya maskini, Kamati ilielezwa kuwa Serikali inaendelea na majadiliano na wafadhali ili kuweza kuanzishwa kwa mradi wa TASAF awamu ya nne. **Ni mtazamo wa Kamati kuwa, Serikali iendelee kuweka juhudi katika kuhakikisha kuwa kunaanzishwa mradi wa kunusuru kaya maskini awamu ya nne, ili kuendelea kuzikwamua kaya zilizo katika hali ya umaskini nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** muhtasari kuhusu upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na fedha za

maendeleo kwa fungu 30 unaoneshwa katika **Jedwali Na. 2** hapa chini.

**Jedwali Na: 2 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi Februari, 2026 - Fungu 30**

| FEDHA | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia ya Mapokezl |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 1,030,823,644,000.00 | 687,215,762,666.67 | 66.67 |
| | Mishahara | 9,016,031,000.00 | 6,194,013,297.00 | 68.70 |
| Jumla Ndogo | | **1,039,839,675,000.00** | **693,409,775,963.67** | **66.68** |
| Maendeleo | Ndani | 88,934,306,000 | 55,661,087,102 | 62.59 |
| | Nje | 68,538,778,000 | 26,093,217,556 | 44.57 |
| **Jumla Ndogo** | | **157,473,084,000** | **81,754,304,657.67** | **55.44** |
| **JUMLA KUU** | | **1,197,312,759,000** | **775,164,080,621.34** | **64.74** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Menenjimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Usanifu wa Kamati.*

## 2.2.3. Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi **74,842,329,000.00** ambapo fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni shilingi **55,086,788,000.00**, kiasi kinachojumuisha mishahara shilingi **18,418,487,000.00** na fedha za matumizi mengineyo (OC)

shilingi **36,668,301,000.00.** Aidha, fedha kwa ajili ya maendeleo zilitengwa shilingi **19,755,541,000.00**, zote zikiwa ni fedha za ndani.

Hadi kufikia Februari, 2026 Fungu 32 lilipokea jumla ya kiasi cha shilingi **44,312,626,616.87** sawa na asilimia **59.21** ya bajeti yote iliyotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa jumla ya shilingi **39,906,392,693.47** sawa na **asilimia 72.44** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Katika kiasi hicho, mishahara ilipokelewa shilingi **12,134,683,224.00** sawa na **asilimia 65.88** ya fedha zilizoidhinishwa ambazo ni shilingi **18,418,487,000.00.** Fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa shilingi **27,771,709,469.47** sawa na **asilimia 75.74** ya fedha zote zilizoidhinishwa ambazo ni shilingi **36,668,301,000.00**

Kwa upande wa fedha za maendeleo, zilipokelewa shilingi **4,406,233,923.40** sawa na **asilimia 22.3** ya fedha za ndani zilizotengwa ambazo ni shilingi **19,755,541,000.00**.

Mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa Fungu 32 unaoneshwa katika **Jedwali Namba 3** hapa chini.

**Jedwali Na: 3 Fedha zilizopokelewa kwa Mwaka wa Fedha Julai, 2025 hadi Februari, 2026) - Fungu 32**

| NA. | Mchanganuo Wa Matumizi | Fedha Iliyoidhinishwa | Fedha Zilizopokelewa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1** | **Fedha za Matumizi ya Kawaida** | | | |
| | Mishahara | 18,418,487,000.00 | 12,134,683,224.00 | 65.88 |
| | Matumizi Mengineyo | 36,668,301,000.00 | 27,771,709,469.47 | 75.74 |
| | **Jumla Ndogo (A)** | **55,086,788,000.00** | **39,906,392,693.47** | **72.44** |
| **2** | **Fedha za Miradi ya Maendeleo** | | | |
| | Fedha za Ndani | 19,755,541,000.00 | 4,406,233,923.40 | 22..30 |
| | Fedha za Nje | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| | **Jumla Ndogo (B)** | **19,755,541,000.00** | **4,406,233,923.40** | **22..30** |
| | **JUMLA KUU** | **74,842,329,000.00** | **44,312,626,616.87** | **59.21** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Menenjimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, fedha za miradi ya maendeleo zimetolewa kwa kiwango kisichoridhisha, kwani zilitolewa **asilimia 22.30** tu badala ya asilimia 66.7 ya kiwango kinachotakiwa kutolewa hadi Februari, 2026. **Kushindwa kutolewa kikamilifu kwa fedha za miradi ya maendeleo, kuna athiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa na wakati mwingine kuongeza gharama za utekelezaji wa miradi husika.**

**2.2.4. Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 16,958,139,000.00.** Kati ya fedha hizo, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni **13,958,139,000.00,** ambapo Katika fedha hizo, Shilingi **3,991,424,000.00** ni mishahara na Shilingi

**9,966,715,000.00** ni Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ni shilingi **3,000,000,000.00.**

**Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Februari 2026, fungu hilo limepokea jumla ya shilingi **9,646,682,702.48**, sawa na **asilimia 56.89** ya fedha zote zilizoidhinishwa ambazo ni shilingi **16,958,139,000.00**. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Shilingi **9,268,479,640.48** ambazo ni sawa na **asilimia 66.4** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikijumuisha Shilingi **2,553,912,490.00** kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **6,714,567,150.48** kwa ajli ya Matumizi Mengineyo.

Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilipokelewa **shilingi 378,203,062.00** sawa na **asilimia 12.61** ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa ambazo ni shilingi **3,000,000,000.00.** Mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa Fungu 33 unaoneshwa katika **Jedwali Namba 4** hapa chini.

**Jedwali 4: Fedha Zilizopokelewa kwa Mwaka wa Fedha Julai, 2025 hadi Februari 2026) - Fungu 33**

| NA. | Mchanganuo Wa Matumizi | Fedha Iliyoidhinishwa | Fedha Zilizopokelewa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Fedha za Matumizi ya Kawaida** | | | |
| | Mishahara | 3,991,424,000.00 | 6,714,567,150.48 | 65.88 |
| | Matumizi Mengineyo | 9,966,715,000.00 | 2,553,912,490.00 | 75.74 |
| | **Jumla Ndogo (A)** | **13,958,139,000.00** | **9,268,479,640.48** | **66.4** |
| 2 | **Fedha za Miradi ya Maendeleo** | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Fedha za Ndani | 3,000,000,000.00 | 378,203,062.00 | 12.61 |
| | Fedha za Nje | 0.00 | - | - |
| | **Jumla Ndogo (B)** | **3,000,000,000.00** | **378,203,062.00** | **12.61** |
| | **JUMLA KUU** | **16,958,139,000.00** | **9,646,682,702.48** | **56.89** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, tathmini inaonesha kuwa, fedha za miradi ya maendeleo zimetolewa kwa kiwango kisichoridhisha, kwani zilitolewa **asilimia 12.61 tu** badala ya **asilimia 66.7**, kiwango kinachotakiwa kutolewa hadi Februari, 2026. Kamati ilielezwa kuwa, fedha za maendeleo zilitengwa kwa lengo la kuanza ujenzi wa Ofisi za kanda za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ikijumuisha kanda ya Nyanda za Juu kusini - Mbeya, Kanda ya Mashariki - Morogoro na kuendeleza ujenzi wa jengo la Kanda ya Ziwa - Mwanza. Hivyo, **Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kikamilifu, kunasababisha changamoto ya kukosekana kwa Ofisi zinazokidhi mahitaji ya wananchi kuwa endelevu, na hivyo kuwakosesha wananchi kupata huduma kwa ufasaha kupitia Ofisi hizo.**

### 2.2.5. Fungu Na. 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi **14,603,888,000.00.** Kati ya fedha hizo, shilingi **13,195,060,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya

kawaida ambapo, mishahara (PE) ni shilingi **2,412,480,000.00** na matumizi mengineyo (OC) ni shilingi **10,782,580,000.00**. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ziliidhinishwa shilingi **1,408,828,000.00**, ambazo zote ni fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika**; hadi kufikia Februari, 2026 fungu 67 limepokea jumla ya shilingi **14,840,888,326.00**, sawa na **asilimia 81.08** ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Katika kiasi kilichopokelewa, shilingi **10,432,060,326.00** sawa na asilimia **79.06** ni fedha za matumizi ya kawaida. Fedha hizo zinajumuisha shilingi **1,869,013,242.68** sawa na asilimia **77.47** ya bajeti kwa ajili ya mishahara iliyoidhinishwa, na shilingi **8,563,047,083.32** sawa na asilimia **79.42** ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za maendeleo, Fungu 67, hadi Februari, 2026 fedha zilizopokelewa ni shilingi **1,408,828,000.00** sawa na asilimia **100** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa bajeti ya fungu hili ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Namba 4** hapa chini.

**Jedwali Na: 4 Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 - Fungu 067**

| Na. | Eneo la Matumizi | Bajeti iliyo Idhinishwa | Fedha zilizopokelewa | % ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA** | Mishahara (PE) | 2,412,480,000.00 | 1,869,013,242.68 | 77.47 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KAWAIDA** | Matumizi Mengineyo (OC) | 10,782,580,000.00 | 8,563,047,083.32 | 79.42 |
| **Jumla** | | **13,195,060,000.00** | **10,432,060,326.00** | **79.06** |
| **MAENDELEO** | Fedha za Ndani | 1,408,828,000.00 | 1,408,828,000.00 | 100 |
| | Fedha za Nje | 0.00 | - | - |
| **JUMLA KUU** | | **14,603,888,000.00** | **11,840,888,326.00** | **81.08** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, mapokezi ya fedha kwa **Fungu 67** ambalo ni Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma kwa mwaka 2025/2026 imekuwa ni ya kuridhisha. Ofisi hii kwa sasa ni muhimu kwa kuwa ndiyo inayosimamia mchakato wa ajira zote katika utumishi wa umma.

lKupokelewa kwa kiasi cha kutosheleza, kitasaidia Ofisi hii kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha, ikiwemo kuendesha usaili wa waombaji wa ajira nchini kwa kutumia mifumo ya TEHAMA. **Ni rai ya Kamati kuwa, kupitia mifumo ya kielekroniki, Ofisi hii ianze kutumia mifumo hiyo kukagua vyeti na vitambulisho mbalimbali pindi wasailiwa wa nafasi mbalimbali za ajira wanapofika kwa ajili ya usahili, badala ya kuwataka watahiniwa hao kubeba vyeti vyao halisia vya elimu pamoja na vitambulisho vyao**.

### 2.2.6. Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utumishi wa Umma katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliidhinishiwa Jumla ya Shilingi **9,677,775,000.00.** Kati ya fedha hizo, shilingi **9,177,599,000.00 ni** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida, zikijumuisha mishahara Shilingi **2,315,295,000.00** na matumizi mengineyo Shilingi **6,862,304,000.00.** Aidha, fedha za miradi ya maendeleo ziliidhinishwa **shilingi 500,176,000.00**.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2026, Fungu 94 lilipokea jumla ya shilingi **7,168,697,115.97,** zote zikiwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida, sawa na Asilimia **78.1** ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, mishahara ni Shilingi **1,609,643,784.00** sawa na asilimia **69.5** ya bajeti ya mishahara, na Matumizi Mengineyo ni Shillingi **5,559,053,331.97** sawa na asilimia **81.0** ya bajeti ya Matumizi Mengineyo. Aidha, hakukuwa na fedha iliyopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti ya fungu hili ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Namba 5** hapa chini.

**Jedwali Na: 5 Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026-Fungu 094**

| Na. | Eneo la Matumizi | Bajeti iliyo Idhinishwa | Fedha zilizopokelewa | % ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | Mishahara (PE) | 2,315,295,000.00 | 1,609,643,784.00 | 81 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **YA KAWAIDA** | Matumizi Mengineyo (OC) | 6,862,304,000.00 | 1,609,643,784.00 | 69.5 |
| **Jumla** | | **9,177,599,000.00** | **7,168,697,115.97** | **78.1** |
| **MAENDELEO** | Fedha za Ndani | 500,176,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| | Fedha za Nje | 0.00 | - | - |
| **JUMLA KUU** | | **9,677,775,000.00** | **7,168,697,115.97** | **74.07** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Usanifu wa Kamati.*

### 2.2.7. Fungu Na. 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **6,150,699,000.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **3,283,404,000.00.**00 ni kwa ajili Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi **1,689,837,000.00** kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **1,177,458,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026, Ofisi hiyo imepokea jumla ya kiasi cha shilingi **3,565,258,346.64**, sawa na **asilimia 57.99** ya kiasi chote kilichoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo. Katika fedha hizo, kiasi cha Shilingi **2,861,786,142.00 ni** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia **46.53** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi cha

fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa zinajumuisha Shilingi **1,096,576,432.00** kwa ajili matumizi ya mishahara (PE) sawa na asilimia **64.89,** na Shilingi **1,765,209,710.50** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) sawa na asilimia **53.76.** Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, zilipokelewa **Shilingi 703,472,204.64** sawa na **asilimia 59.74** ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla hali ya utekelezaji wa bajeti kwa fungu hili (Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa) ilikuwa ya wastani, kwani ilifikia **asilimia 57.99** badala ya **asilimia 66.7**, kiasi kinachopaswa kufikiwa hadi februari, 2026. Hata hivyo, fedha za matumizi ya kawaida upatikanaji wake ulikuwa chini zaidi, kwani ilipokelewa **asilimia 46.53**. Kutokupatikana kwa fedha hizo kwa kiasi kinachotosheleza, kuna athiri utekelezaji mzuri wa kazi za taasisi hii muhimu nchini.

## 2.3 Tathmini ya Jumla ya Utekelezaji wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla ni wa kuridhisha, hususani kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, hali haikuwa nzuri kwa baadhi ya mafungu ya Ofisi hiyo.

Kamati imebaini kuwa, licha ya Ofisi kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **183,315,087,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi imepokea **Shilingi 88,651,041,847.71** pekee sawa na **asilimia 48.36** ya fedha zilizoidhinishwa kiasi hicho ni chini ya matarajio.

Kutokana na hali hiyo, **Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji wa fedha za maendeleo katika kipindi kilichobaki cha mwaka wa fedha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyopangwa kufanyika kwa wakati, kuepusha kuchelewa kwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo, na kuhakikisha thamani ya fedha pamoja na malengo yaliyokusudiwa kwa wananchi yanafikiwa ipasavyo**.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 6** na **Jedwali Na. 7** hapa chini.

**Jedwali Na: 6 Upatikanaji wa bajeti ya Matumzi ya Kawaida kwa mafungu yote**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2025/2026 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 34,804,735,000.00 | 23,287,471,936.00 | 66.91 |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la | 1,039,839,675,000.00 | 693,409,775,963.67 | 66.68 |

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2025/2026 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| Mawaziri | | | |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 55,086,788,000.00 | 39,906,392,693.47 | 72.44 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 13,958,139,000.00 | 9,268,479,640.48 | 66.4 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 13,195,060,000.00 | 10,432,060,326.00 | 79.06 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 9,177,599,000.0 | 7,168,697,115.97 | 78.1 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 4,974,241,000.00 | 2,861,786,142.50 | 57.54 |
| **JUMLA KUU** | **1,171,035,237,000.00** | **786,334,663,818.09** | **67.15** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2026.*

**Jedwali Na: 7 Upatikanaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mafungu yote kwa Mwaka 2025/2026**

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 157,473,084,000.00 | 81,754,304,657.67 | 55.44 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala | 19,755,541,000 .00 | 4,406,233,923.40 | 22.3 |

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | |
| Bora | | | |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 3,000,000,000.00 | 378,203,062.00 | 12.61 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 1,408,828,000.00 | 1,408,828,000.00 | 100 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 500,176,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 1,177,458,000.00 | 703,472,204.64 | 59.74 |
| **JUMLA KUU** | **183,315,087,000.00** | **88,651,041,847.71** | **48.36** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2026.*

## 2.4 Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua jumla ya miradi sita (6) inayotekelezwa na Wizara hii iliyopo katika mikoa ya Geita na Mwanza. Uchambuzi kuhusu miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

### 2.4.1. Miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) -Mradi Na. 6220.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikagua jumla ya miradi miwili inayotekelezwa na TASAF iliyopo katika halmashauri ya jiji la Mwanza. Miradi hiyo ni:-

a) **Ujenzi wa Kiwanda cha Kutengeneza Siagi ya Karanga – Ilemela Kabangaja.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianza kutekelezwa Agosti, 2024 unatekelezwa na kikundi cha wanawake kiitwacho **Wasikivu**. Kikundi hiki cha Wanawake kinajishughulisha na kazi ya kusaga karanga, kutengeneza sabuni za maji, sabuni za miche na unga wa lishe.

**Mheshimiwa Spika**; Mradi huu ulitengewa kiasi cha Shilingi **11,596,250.00**, kwa ajili ya utekelezaji. Kamati ilielezwa kuwa Mradi huu unatekelezwa kwa wanufaika 15 ambao ni walengwa na Wakazi wa Kabangaja, kata ya Bugogwa Manispaa ya Ilemela kupitia Mpango wa Kupunguza Umaskini Awamu ya Nne (TPRP) kupitia TASAF Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2026 wakati Kamati ilipofanya ziara ya ukaguzi wa Miradi, Mradi ulikuwa umepokea kiasi cha shilingi** 11,594,868.48 **sawa na** asilimia 99.98 **ya gharama ya mradi. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa mradi huo umekamilika na tayari wanakikundi wananufaika na ujuzi walioupata kupitia SIDO kwa kuzalisha bidhaa za kibiashara, kuziuza sokoni na hivyo kujipatia kipato cha ziada kinachochangia kuboresha hali yao ya kiuchumi**

**b) Ujenzi wa Zahanati – Ilemela (Mihama) (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mradi ulipokea kiasi cha **Shilingi 232,287,214.00,** kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 118,196,205.00** kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya mganga, jengo la ukunga, na vyoo matundu manne (4), na Shilingi **114,091,009.00** kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) ambao utawawezesha walengwa kupata huduma za afya kwa haraka zaidi na kupunguza umbali wa kuitafuta huduma hiyo.

**Mheshimiwa Spika**; Mradi huo umekamilika kwa **asilimia 100** ukiwa umeshatumia kiasi cha Shilingi **232,285,249.36** sawa na **Asilimia 99.99** ya fedha iliyoidhinishwa. Aidha, kamati ilielezwa kuwa mradi

umekabidhiwa kwa serikali ya kijiji chini ya uangalizi wa Kata ya Mihama.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kukagua mradi huu na kukutana na wanufaika wa TASAF, kamati ilipokea shukrani za dhati zilizoelekezwa kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuboresha miundombinu ya afya nchini.
Aidha, Kamati ilibaini kuwa changamoto ya miundombinu mibovu ya vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na umbali mrefu wa wananchi kufuata huduma hizo ilikuwa ikisababisha ugumu wa upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi. Hivyo, Kamati inaona mradi huu kuwa na tija kubwa kwa Taifa na inaipongeza Serikali pamoja na Wananchi wa kata ya Mihama kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo.

### 2.4.2. Ujenzi wa Jengo la Ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nyangh'wale-Mradi Na. 6203:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mradi ulipokea kiasi cha **Shilingi 385,404,150.00.** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Hadi kukamilika kwa kazi zote kwa mujibu wa mawanda ya mradi, kimetumika kiasi cha **Shilingi**

**386,038,051.67** ikiwa ni ongezeko la **Shilingi 633,901.67** sawa na ongezeko la asilimia 0.16 ya bajeti ya mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliambiwa kuwa, Mradi huu ulikamilika tarehe 3 Oktoba, 2025 ukiwa umechelewa kwa siku 47 kutoka kwenye muda wa mkataba uliokuwa umepangwa kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya vifaa vya ujenzi kutokupatikana wilayani Nyang'hwale.

Changamoto hii ilisababisha Mradi huu kuongezewa muda na kuongeza gharama za usafirishaji ambapo vifaa vingi vilinunuliwa kutoka Mjini Geita, Manispaa ya Kahama na Jijini Mwanza.

Aidha, Mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 ukiwa umeshatumia kiasi chote cha fedha. Kamati iliridhika na inaipongeza Serikali kwa ubora na thamani ya fedha (Value for Money) katika Mradi huo wa Nyangh'wale. Ni imani ya Kaamati kuwa Mradi huo utaiwezesha Ofisi hii katika Mapambano dhidi ya Rushwa.

### 2.4.3. Ujenzi na Ukarabati wa Jengo la Ofisi na Ghala Kuu la Nyaraka, Ilemela (Mradi Na. 6286 na Mradi Na. 6285)

**Mheshimiwa Spika**; Mradi huu unatekelezwa na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – Fungu 004.

Kamati ilielezwa kuwa, Ujenzi wa Kituo hiki ulianza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na ulikamilika katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ukitekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Mradi ulihusu ujenzi wa majengo tu, ambapo vifaa na miundombinu mingine ya Kituo imekuwa ikiombewa fedha kila Mwaka wa Fedha ili kukifanya Kituo hicho kuwa kamili kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Hata hivyo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Kituo kiliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 233,319,000.00** kwa ajili ya kununua mashubaka, kuweka mfumo wa udhibiti wa usalama wa maghala ya kuhifadhia nyaraka, ununuzi wa *Heavy Duty Scanner* na uwekaji mfumo wa CCTV Camera.

Vilevile Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Februari, 2026 Kituo kilipokea jumla ya **Shilingi 212,641,050.80** sawa na **asilimia 91** ambazo zilitumika kunununua mashubaka, kufunga mfumo wa udhibiti wa usalama wa maghala, ununuzi wa *heavy duty scanner mbili* na ufungaji wa CCTV Camera.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umekamilika kwa Asilimia 91 ikiwa imetumia kiasi chote cha fedha kilichopokelewa.
Aidha, Kamati ilibaini kuwa kituo kinakumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo Ufinyu wa bajeti kwa ajili

ya kuwezesha kazi ya ukusanyaji na uhifadhi wa kumbukumbu; Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha na kutozingatiwa kwa Sheria, Taratibu na Miongozo ya utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma; kutokuwa na ulinzi wa Jeshi la Polisi hivyo, kuhatarisha usalama wa taarifa na nyaraka za Serikali; na Ubovu wa barabara ya kuingilia Kituoni kutokea barabara kuu inayoelekea Ilemela.

Hata hivyo, mradi huu una tija kwa Taifa na Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo kwani baada ya kukamilika kwake kituo kitaunganishwa na mifumo ya Serikali Mtandao (*e-Government*) hivyo kukiwezesha kituo kutunza kumbukumbu za kidigitali kutoka Makao Makuu ya Idara ili kuwa na hifadhi mbadala (*back up)* kwa ajili ya usalama wake.

### 2.4.4. Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Jengo la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

**Mheshimiwa Spika**; Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Mradi huu uliidhinishiwa kiasi cha shilingi **3,000,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji. Hadi kufikia Februari, 2026 Jumla ya shilingi **378,203,062.00** sawa na **asilimia 12.6** zilipokelewa na kutumika.

**Mheshimiwa Spika**; Kamati iliambiwa kuwa, Ujenzi Mradi huu umefikia asilimia 41. Kwa hatua hii Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati uliopangwa kwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi pamoja na upatikanaji wa fedha kwa wakati ili kuepuka ongezeko la gharama na kuchelewesha kuanza kutumika kwa ofisi hiyo.

### 2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo Matano (5). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, tarehe 24 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni makadirio ya mapato na matumizi katika matumizi ya kawaida na matumizi ya

maendeleo. Tathmini ya uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

## 3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ifuatavyo: -

### 3.1.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Ofisi Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,402,593,992,000.00** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **asilimia 19.77** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Shilingi 1,171,036,237,000.00.**

Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kuongezeka kwa watumishi, kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika;** Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika kwa ufanisi, uwajibikaji na kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa. Ili kuhakikisha utekelezaji huu unafanyika ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya fedha hizo.

Aidha; Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inawasilisha kwa wakati mbele ya Kamati taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria, zikiwa na taarifa za kina kuhusu matumizi halisi ya fedha, viwango vya utekelezaji wa miradi, pamoja na changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa kuzitatua.

Sambamba na hilo; Kamati inapendekeza Serikali kuweka viashiria mahsusi vya kupima utendaji (performance indicators) ili kurahisisha tathmini ya thamani ya fedha (value for money) katika miradi inayotekelezwa. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 8** hapa chini.

**Jedwali Na: 8 Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2025/2026 na Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2026/2027**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO YA FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | ASILIMIA YA ONGEZEKO/UPUNGUFU (-) |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 34,804,735,000.00 | 39,416,152,000.00 | 13.25 |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 1,039,839,675,000.00 | 1,256,299,943,000.00 | 20.82 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 55,086,788,000.00 | 55,832,858,000.000 | 1.35 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 13,958,139,000.00 | 15,074,774,000.00 | 7.99 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 13,195,060,000.00 | 17,883,739,000.00 | 35.53 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 9,177,599,000.00 | 12,354,903,000.00 | 34.62 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 4,973,241,000.00 | 5,731,623,000.00 | 15.25 |
| **JUMLA KUU** | **1,171,035,237,000.00** | **1,402,594,992,000.00** | **19.77** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2026.*

### 3.1.2 Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 163,000,008,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 161,770,018,000.00** ni fedha za ndani, na **Shilingi 1,229,990,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepungua kwa **Sh. 20,315,079,000.00** sawa na **asilimia 12.46** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 9**

**Jedwali Na: 9 Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| FUNGU | MAKADIRIO YA FEDHA YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | MAKADIRIO YA FEDHA YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | ASILIMIA YA ONGEZEKO /UPUNGUFU (-) |
|---|---|---|---|
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 157,473,084,000.00 | 126,638,005,000.00 | 19.58 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 19,755,541,000.00 | 29,055,541,000.00 | 47.08 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 3,000,000,000.00 | 3,000,000,000.00 | 0.00 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 1,408,828,000.00 | 1,408,828,000.00 | 0.00 |

| FUNGU | MAKADIRIO YA FEDHA YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | MAKADIRIO YA FEDHA YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | ASILIMIA YA ONGEZEKO /UPUNGUFU (-) |
|---|---|---|---|
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 500,176,000.00 | 500,176,000.00 | 0.00 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 1,177,458,000.00 | 2,397,458,000.00 | 103.61 |
| **JUMLA KUU** | **183,315,087,000.00** | **163,000,008,000.00** | **11.08** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2026.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani, jambo linalodhihirisha dhamira ya Serikali ya kuimarisha uwezo wa ndani katika kugharamia maendeleo na kupunguza utegemezi wa vyanzo vya nje vya fedha.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

## 4.1 MAONI YA JUMLA

i) Serikali ihakikishe fedha zinazoidhinishwa zinatolewa kwa wakati na kwa kiwango stahiki ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli na miradi iliyopangwa kufanyika kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya yaliyokusudiwa;

ii) Serikali iongeze juhudi katika usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha zinazoidhinishwa ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa ufanisi, kuleta tija na kwa kuzingatia thamani ya fedha katika utekelezaji wa shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa; na

iii) Serikali iboreshe mfumo wa kufanya usaili kwa njia ya mtandao *(Online Aptitude Test – OATS)* kwa kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na huduma za mtandao ili kuondoa changamoto za kukatika au kusuasua kwa mfumo wakati wa usaili.

## 4.2 Ushauri Mahsusi Fungu kwa Fungu

### 4.2.1 Fungu 30- Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

#### (a) Maoni Kuhusu TASAF

Serikali kupitia TASAF inashauriwa kwamba, inapopanga na kuratibu shughuli za kijamii zinazowahusu wananchi, ihakikishe inashirikiana kwa karibu na viongozi wa maeneo husika, wakiwemo Wabunge, ili kuongeza ushiriki wa viongozi katika shughuli hizo na kuimarisha mshikamano na uwajibikaji kwa jamii.

#### (b) Maoni Kuhusu TAKUKURU

i) Vijiji vilivyofanyiwa mafunzo na Mradi wa TAKUKURU Rafiki (BSAAT) vifanyike Mfano kwa vijiji vingine ili kuendana na Falsafa ya 4R za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo ni Maridhiano (Reconciliation), Ustahimilivu (Resiliency), Mabadiliko (Reforms) na Kujenga upya (Rebulding) katika ngazi za vijiji;

ii) TAKUKURU ijenge nyumba za makazi kwa watumishi wake ili kuwaondolea watumishi hao utegemezi wa kupanga katika mazingira yanayoweza kusababisha mgongano wa

kimaslahi (conflict of interest), na hivyo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa uhuru, weledi na ufanisi zaidi;

iii) TAKUKURU iongeze kasi ya ujenzi wa ofisi katika Wilaya na Mikoa mbalimbali hususani maeneo mengine ya Kimkakati;

**(c) Moani Kuhusu Mamlaka ya Serikali Mtandao – e-GA**

Kutokana na uwepo wa mifumo mingi ya kielektroniki inayosababisha changamoto katika matumizi yake kwa watumiaji, Serikali kupitia Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) ihakikishe inaunganisha mifumo yenye ufanano wa matumizi na majukumu ili kupunguza changamoto ya kuwa na mifumo mingi inayohitaji nywila tofauti tofauti na kurahisisha matumizi kwa watumiaji.

### 4.2.2 Fungu 67-Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Serikali iboreshe mfumo wa ajira kwa kuruhusu waombaji wenye sifa na vyeti vya ngazi mbalimbali kushiriki katika usaili wa nafasi za kazi zinazotangazwa pindi zinapojitokeza, bila kuwekewa vikwazo visivyo vya lazima kwa misingi ya kiwango cha elimu pekee. Hatua hiyo itaondoa malalamiko ya kuwanyima wasomi mbalimbali fursa ya kuomba na kupata ajira mbalimbali kulingana na aina ya elimu waliyonayo kadiri watakavyoona inafaa kwa kuwa kwa

kutumia baadhi ya vyeti vyao wanatimiza vigezo na masharti yaliyobainishwa katika tangazo la ajira husika.

### 4.2.3 Fungu Na. 004-Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Kwa kuzingatia kuwa vituo husika havina ulinzi wa uhakika ilhali vinatunza taarifa nyeti na muhimu kwa maslahi ya Taifa, Serikali itenge bajeti mahsusi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika vituo vyote, ikiwemo kufunga mifumo ya tahadhari na kinga dhidi ya majanga ya moto, ili kuhakikisha usalama wa vituo hivyo na ulinzi wa taarifa hizo wakati wote.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb | - | **M/Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb | - | **Mjumbe** |
| 4. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | - | **Mjumbe** |
| 5. | Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb | - | **Mjumbe** |
| 6. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb | - | **Mjumbe** |
| 7. | Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb | - | **Mjumbe** |
| 8. | Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb | - | **Mjumbe** |
| 9. | Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb | - | **Mjumbe** |
| 10. | Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb | - | **Mjumbe** |
| 11. | Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb | - | **Mjumbe** |
| 12. | Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb | - | **Mjumbe** |
| 13. | Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 14. | Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb | - | **Mjumbe** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 16. | Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 17. | Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb | - | **Mjumbe** |
| 18. | Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb | - | **Mjumbe** |
| 19. | Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 20. | Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb | - | **Mjumbe** |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru **Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb)** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa ambao ameendelea kuipa Kamati pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Regina Ndege Qwaray.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo Ndg. Juma Selemani Mkomi Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ndg. Majula Mahendeka Katibu Mkuu Ikulu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru

Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.



Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**

**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

17 Aprili, 2026